



UKWELI WA HARAKA: CHANJO ZA COVID-19 NA UJAUZITO

Kuna maelezo mengi yasiyo ya ukweli kuhusu Chanjo za COVID-19 na ujauzito. Acha tutatue baadhi ya ukweli unaojulikana!

Chanjo za COVID-19 ni salama kabla ya, wakati wa, na baada ya, ujauzito.

Chanjo wakati wa ujauzito inapendekezwa na College of Obstetricians and Gynecologists (ACOG, Chuo cha Wakunga na Wanajinokolojia) cha Marekani na Centers for Disease Control and Prevention (CDC, Vituo vya Udhhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa) ili kutoa ulinzi dhidi ya maradhi makali ya COVID-19.

Watu wajawazito wapo katika hatari ya juu ya maradhi makali na matatizo makali iwapo wataambukizwa COVID-19.

Kuugua sana COVID-19 wakati wa au baada ya ujauzito unaweza kuongeza pakubwa hatari ya kulazwa hospitalini ya kuhitaji kipumuzi, matatizo wakati wa ujauzito, kuzaa kabla ya wakati, au kuzaa mtoto aliyekufa.

Hakuna ushahidi wa kupendekeza chanjo za COVID-19 husababisha matatizo ya kuzaliwa, kuavya mimba, kuzaa kabla ya wakati kufika, kuzaa mtoto aliyekufa, au matatizo mengine.

Hata hivyo, maradhi ya COVID-19 yanajulikana kuwa huwa yanasababisha matatizo haya.

Ni salama kupokea chanjo iwapo unanyonyesha.

Maziwa ya mama yanaweza kuhamisha kingamaradhi kwenda kwa mtoto wako ili kusaidia kuwalinda dhidi ya maambukizo ya COVID-19 hadi atakapostahiki kupokea chanjo atakapofikisha umri wa miezi 6.

Rasilimali:

[Chanjo za COVID-19 Ukiwa Mjamzito au Unaponyonyesha \(cdc.gov\)](https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/recommendations/pregnancy.html) | <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/recommendations/pregnancy.html> (Kiingereza, Kihispania, Kikorea, Kivietnamu, na Kichina pekee)

[Watu Wajawazito na Waliokuwa Wajawazito Hivi Karibuni | CDC](https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/need-extra-precautions/pregnant-people.html) | <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/need-extra-precautions/pregnant-people.html> (Kiingereza pekee)

[Chanjo ya COVID-19 na Ujauzito: Unachohitaji Kujua | Johns Hopkins Medicine](https://www.hopkinsmedicine.org/health/conditions-and-diseases/coronavirus/the-covid19-vaccine-and-pregnancy-what-you-need-to-know) | <https://www.hopkinsmedicine.org/health/conditions-and-diseases/coronavirus/the-covid19-vaccine-and-pregnancy-what-you-need-to-know> (Kiingereza pekee)